

Nambari ya Mtahiniwa _____
SMZ

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA

125

URAIA

MUDA: Saa 2.00

JUMATANO 22 NOVEMBA, 2017 mchana

MAELEKEZO KWA WATAHINIWA

- 1. Mtihani huu una sehemu TATU (3) A,B na C.**
- 2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B; na maswali MANNE (4) kutoka sehemu C.**
- 3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
- 4. Jawabu zote ziandikwe katika nafasi zilizowekwa.**
- 5. Simu za mkononi haziruhusiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

KWA MATUMIZI YA USAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
11.		
JUMLA		

Mtihani huu una kurasa 24 zenye maandishi

Nambari ya Mtahiniwa

SEHEMU A: (Alama 20)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii

1. Chagua jawabu sahihi kisha andika herufi ndani ya jadweli liliopo hapo chini.
 - i) Moja ya kati ya misingi ya demokrasia ni
 - A. Utawala wa kidikteta
 - B. Utawala wa sheria
 - C. Utawala wa mabavu
 - D. Utawala wa upendeleo
 - ii) Kipengele gani kinahusiana na uvunjaji wa sheria za nchi?
 - A. Kufanya kazi kwa bidii
 - B. Kutojichukulia sheria mikononi
 - C. Kujichukulia sheria mikononi
 - D. Kufuata mafundishio ya dini
 - iii) Baraza la Wawakilishi huongozwa na
 - A. Wabunge
 - B. Rais
 - C. Spika
 - D. Mawaziri
 - iv) Sifa moja ya mgombea ujumbe wa Baraza la Wawakilishi ni
 - A. Kuwa na uraia wa nchi nyengine
 - B. Kuwa si mgombea aliependekezwa na chama
 - C. Kuwa Mzanzibari aliyetimia umri wa miaka 21
 - D. Kuwa Mzanzibari aliyetimia umri wa miaka 18
 - v) Lengo mojawapo la kuanzishwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni
 - A. Kujihusisha na uhifadhi wa mazingira
 - B. Kuishi kwa tahadhari muda wote
 - C. Kuendeleza uhusiano wa kimichezo
 - D. Kuwa na mfumo sawa wa ushuru

Nambari ya Mtahiniwa

- vi) Watu wanapozungumzia Rushwa husema Rushwa ni
- A. Adui wa jamii
 - B. Adui wa haki
 - C. Adui kwa mtu binafsi
 - D. Huduma kwa haraka
- vii) Zifuatazo ni kazi za J.K.U isipokuwa
- A. Kujiunga na vikosi vyingine vya ulinzi na usalama
 - B. Kutoa huduma za ulinzi kwa taasisi za umma au za binafsi
 - C. Kushirikiana na jeshi la wananchi wa Tanzania
 - D. Kulinda maliasili za baharini
- viii) Moja kati ya faida za utandawazi ni
- A. Kupungua kwa idadi ya watu
 - B. Kumog'onyoka kwa maadili
 - C. Kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano
 - D. Kudidimia kwa lugha ya Kiswahili
- ix) Umoja wa Afrika uliazishwa tarehe
- A. 10/07/2002 B. 10/05/2000
 - C. 09/09/ 1999 D. 25/05/1963
- x) Zifuatazo ni kazi za Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania isipokuwa
- A. Kutunga sheria
 - B. Kujadili na kuridhia mikataba
 - C. Kujadili utekelezaji wa kila wizara
 - D. Kuitisha uchaguzi mkuu

JAWABU

i	ii	iii	iv	v	vi	vi	viii	ix	x

Nambari ya Mtahiniwa

2. Andika "Kweli" mbele ya maelezo yaliyo sahihi na "Sikweli" mbele ya maelezo yasiyo sahihi.

- i) Utawala bora ni utaratibu wa kufanya maamuzi unaozingatia sheria na kanuni za nchi. _____
- ii) Uchaguzi ulio huru na wa haki ni msingi wa kidemokrasia. _____
- iii) Katiba iliyoandikwa huwa na nyaraka nyingi. _____
- iv) Kazi ya serikali ya wilaya ni kutoa huduma bora kitaifa. _____
- v) Uchumi wa soko huria ni nyanja ya utandawazi. _____
- vi) Kukuza umoja na mshikamano miongoni mwa wanachama ni changamoto ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. _____
- vii) Muathirika wa Ukimwi hana haki ya uhuru na usalama. _____
- viii) Ulinzi na usalama wa Taifa husimamiwa na Baraza la Mawaziri _____
- ix) Mahakama zinapaswa kufanya kazi zake kwa upendeleo. _____
- x) Kazi ya Idara ya Uhamiaji ni kutoa hati ya ukaazi kwa wageni. _____

SEHEMU B: (Alama 40)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii

3. Chagua maelezo sahihi kutoka KIFUNGU B yanayokubaliana na maelezo ya KIFUNGU A.

KIFUNGU A	KIFUNGU B
i. Kuongezeka kwa tofauti ya mapato	A. Umoja wa Mataifa
ii. Kuporomoka kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki	B. Aina ya demokrasia
iii. Demokrasia ya moja kwa moja	C. Athari za utandawazi
iv. TISS	D. 2000
v. Jumuiya inayoziunganisha nchi huru zote Duniani	E. Tanzania Institute of Security Services
	F. Tanzania Intelligence and Security Services
	G. 1977
	H. Umoja wa nchi za Afrika
	I. Umoja wa Ulaya

Nambari ya Mtahiniwa

	J. 1967
--	---------

JAWABU

i	ii	iii	iv	v

4. Jaza nafasi zilizo wazi katika sentensi zifuatazo.

- a) Ukimwi husababishwa na vijidudu vidogo vyenye uhai vinavyoitwa _____
- b) Dawa za kulevya huleta athari kwa afya ya mtumiaji na _____
- c) Mahakama ni chombo chenye kutafsiri _____
- d) Wajibu wa raia ni kuheshimu sheria na _____ za nchi.
- e) Mwanasheria Mkuu ni mshauri wa Serikali kuhusu mambo ya _____

5. Jibu maswali yafuatayo kwa ufupi.

- a) Nini maana ya haki za binadamu?

Nambari ya Mtahiniwa _____

b) Andika faida mbili (2) wanazopata Tanzania katika Umoja wa Afrika .

c) Taja miiko miwili (2) ya kiongozi bora.

d) Ainisha athari mbili (2) za ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia.

e) Chora mchoro unaoonesha mgawanyiko wa vyombo vikuu vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

SEHEMU C: (Alama 40)

Nambari ya Mtahiniwa _____

Jibu maswali MANNE (4) tu katika sehemu hii

6. Elezea hasara nne (4) za mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini Tanzania.

7. a) Unafahamu nini kuhusu Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika?

b) Taja taasisi nne (4) muhimu za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

Nambari ya Mtahiniwa

8. Elezea changamoto tano (5) za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

9. a) Serikali ya Mkoa inaundwa na vyombo vingi, taja vinne (4) kati ya vyombo hivyo.

- b) Elezea kazi tatu (3) za Serikali ya Mkoa.

Nambari ya Mtahiniwa _____

10. Bainisha mambo matano (5) yanayoweza kujuulisha kuwa watu wanatii sheria za nchi ipasavyo.

11. a) Andika kirefu cha JWTZ.

- b) Nini lengo la kuanzishwa kwa JWTZ?

- c) Eleza kazi tatu (3) za JWTZ.

Nambari ya Mtahiniwa_____

This image shows a single sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

=====